

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI



### **TANGAZO KWA UMMA**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemevu anakaribisha maombi ya vijana kuijunga na mafunzo kwa njia ya vitendo (Incubation) kuhusu utengenezaji wa vizimba nya samaki; utengenezaji wa boti za ute kioo (fibre boats); utengenezaji wa chakula cha samaki; ufügaji wa samaki kwenye vizimba; ufügaji wa majongoo bahari, unenepeshaji kaa na kilimo cha mwani; uchakataji wa samaki; uzalishaji wa vifaranga nya samaki pamoja na ujasiriamali yatakayogharamiwa na Serikali.

#### **1. Sifa za Mwombaji**

- i. Mwombaji awe kijana wa kitanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18);
- ii. Awe amehitimu fani za uvuvi na ukuzaji viumbe maji au mwenye nia ya kujishughulisha na uvuvi na ukuzaji viumbe maji;
- iii. Awe tayari kupata mafunzo kwenye mikoa na vituo vilivyoteuliwa; na
- iv. Awe tayari kujitegemea kwa malazi na chakula.

#### **2. Muda wa Mafunzo: -**

Mafunzo yatatolewa na Serikali kwa muda wa miezi mitatu (**3**) katika Mikoa ya kanda ya Ziwa Victoria na Pwani. Nafasi zilizopo kwa ajili ya mafunzo hayo ni **mia tatu (300)** tu. Aidha, Serikali itatoa **kiasi cha shilingi 150,000/= kwa kila mshiriki kwa mwezi.**

#### **3. Jinsi ya kutuma Maombi**

- i. Barua ya maombi iambatanishwe na nakala ya vyeti pamoja na wasifu (CV);
- ii. Maombi yote yatumwe kwa **Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, S.L.P 2847, Mji wa Serikali, Mtumba, Mtaa wa Ulinzi 40487-Dodoma** na kuwasilishwa kuititia barua pepe [barua@uvuvi.go.tz](mailto:barua@uvuvi.go.tz)
- iii. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 09 Agosti, 2023 saa 9:30 Alasiri.
- iv. Kwa maelezo zaidi wasiliana 0717 369 588/0655 669 942/0788 648 643.

**Imetolewa na:**

**KATIBU MKUU**